Mwongozo Wa Mwanafunzi

5

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

## Kuonekana mwenye mafanikio machoni pa Mungu



MVMM

Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

## Kuonekana mwenye mafanikio machoni pa Mungu

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwanafunzi

Toleo la Tano

Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

## Kuonekana mwenye mafanikio machoni pa Mungu

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwanafunzi

Toleo la tano

Maandiko yanayotumiwa katika kitabu hiki yametoka kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwa mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bila malipo. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *Successful Christian Living, 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, shuleni, katika huduma gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, kitabu cha kuongoza mafunzo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.org na
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 08-2023

# Yaliyomo

Utangulizi ..............................................................................................4

**Sura ya 1. Mimi ni nani? ..............................................................................5**

A. Kile Mungu anasema kunihusu ..............................................................5

B. Niko na mwili halisi ..............................................................................7

C. Niko na utu ..........................................................................................8

D. Niko na roho ........................................................................................10

**Sura ya 2. Hatua tano za kuwa Mkristo aliyefanikiwa ....................................11**

A. Je! Hatua hizi Tano ni Zipi? ..................................................................11

Hatua ya 1. Kuwa Mkristo ........................................................................12

Hatua ya 2. Badilisha jinsi unavyofikiria ....................................................13

Hatua ya 3. Weka malengo mapya ..............................................................14

Hatua ya 4. Jifunze jinsi ya kudhibiti hisia zako ..........................................19

Hatua ya 5. Wafahamishe wengine kile Kristo amefanya katika maisha yako ..........22

B. Jinsi ya kuanza kutumia hatua hizi tano ....................................................23

**Sura ya 3. Roho Mtakatifu ..........................................................................26**

A. Roho Mtakatifu ni nani? ........................................................................26

B. Je! Roho Mtakatifu hufanya nini katika maisha yako unapokuwa Mkristo? ..........27

C. Roho Mtakatifu hufanya nini katika maisha yako baada ya wewe kuwa Mkristo? ..........29

# Utangulizi

Leo hii tunasikia mazungumzo mengi yanayohusu mafanikio. Pesa ni njia mojawapo ya kawaida ya kupima mafanikio. Ikiwa unazo nyingi, basi ulimwengu husema umefanikiwa. Viongozi wa kisiasa wanaoshinda uchaguzi huhesabiwa kama mafanikio. Kwao, ufanisi mkubwa ni ikiwa watatunga sheria na kuwa na mipango inayosaidia watu kuwa na mafanikio zaidi.

Kozi hii haishugulikii kile ambacho ulimwengu unasema ni mafanikio. Tunataka kuchunguza kile Mungu anasema juu ya mafanikio na jinsi tunaweza kuwa Wakristo waliofanikiwa. Mungu hupima mafanikio kwa njia tofauti sana na watu matajiri na wenye nguvu ambao sio Wakristo. Wakati Mungu anapoangalia maisha yako, atasema nini? Je! Anakuona kama mtu aliyefanikiwa kulingana na mtazamo wake? Je, ni nini anachoweza kuona ndani yako ili aweze kukuambia, “Ninajivunia wewe. Wewe ni Mkristo aliyefanikiwa sana”?

Biblia imejaa mafundisho mengi na vielelezo vingi vya kutuonyesha jinsi Mungu anavyoona mafanikio. Katika kozi hii tutajadili jinsi unavyoweza kuwa Mkristo aliyefanikiwa. Kuanzia mwanzo kuna kweli mbili za msingi tunazohitaji kujifunza. Kwanza, sio lazima uwe mkamilifu kabla ya Mungu kusema wewe ni Mkristo aliyefanikiwa. Ingawa unaweza kufeli, hii haimaanishi kwamba Mungu anatakuacha.

Pili, Roho Mtakatifu ndiye pekee anayeweza kukupa nguvu ambazo unahitaji kuwa Mkristo aliyefanikiwa. Haiwezekani kumpendeza Mungu kwa nguvu zako mwenyewe. Tuna kila sababu ya kuwa na furaha, kwa sababu Mungu ameahidi kuwa nasi na kutupatia nguvu tunayohitaji kuishi kwa ajili Yake.

Katika Sura ya 3 ya kozi hii, tutaangalia kwa karibu jinsi Roho Mtakatifu anavyohusika kibinafsi kukusaidia kuwa Mkristo aliyefanikiwa.

# Sura ya 1
# Mimi ni nani?

Je! Umewahi kujiuliza wewe unafanana na nani? Sio mwili wako wa asili, lakini wewe halisi, ndani kabisa. Mungu alituumba kwa mpango kwamba sote tuwe watu kamili. Ikiwa tutakuwa Wakristo waliofaulu, tunahitaji kuelewa sisi ni nani.

Ikiwa utatumia vipimo vya ulimwengu vya urembo wa mwili, pesa, na nguvu ili kuelewa wewe ni nani, basi inaweza kuwa rahisi kwako kukata tamaa. Unapotazama siku zako zilizopita, unaweza kukata tamaa kutokana na makosa makubwa na makosa na kufeli ambayo ulifanya.

Katika Biblia, Mungu anasema mambo kadhaa juu ya jinsi alivyotuumba. Wacha tuangalie kwa undani kile anachofikiria kukuhusu.

## A. Kile Mungu anasema kunihusu

Mungu anataka kuwa na uhusiano wa karibu na wa kibinafsi na wewe. Mtu ambaye si Mkristo ana uhusiano uliovunjika na Mungu. Vifaa vifuatavyo katika sehemu hii vimeandikwa kutoka kwa mtazamo kwamba wewe ni Mkristo.

Ikiwa bado haujafanya uamuzi wa kuwa Mkristo, basi soma hii na ujiulize swali, “Je! Hivi ndivyo ninavyotaka Mungu anione wakati Ananitazama?”

### 1. Mimi ni mtoto wa Mungu

Mungu anakuona kama mtu wa familia yake! Wewe ni mtoto wake. Tazama Yohana 1:12 na Waefeso 1:4-5.

### 2. Mimi ninapendwa-Mungu ananipenda!

Mungu anakuopenda zaidi ya kitu kingine chochote. Upendo wake ni halisi, safi, salama, na ambao hauna nia iliyofichwa. Tazama Yohana 3:16 na 1 Yohana 3:1.

### 3. Mimi ni wa thamani

Mungu anasema wewe ni wa thamani. We ni wa thamani zaidi kuliko utajiri wote wa ulimwengu. Tazama Luka 15:7-10 na Mathayo 6:26. Wakati Yesu alikufa msalabani ili kulipa adhabu ya dhambi zako, Alionyesha wazi ni kwa kiasi gani Anakujali. Alifanya yote hayo ili uwe rafiki yake na kuishi naye milele mbinguni.

## 4. Mimi ni mtu aliyenunuliwa

Kabla ya wewe kuwa Mkristo, ulikuwa mtumwa wa dhambi, mwenye hatia na mfungwa wa kuzimu. Lakini Yesu alinunua uhuru wako. Tazama 1 Wakorintho 6:19-20.

## 5. Mimi ni mtumwa (mfuasi) wa Yesu Kristo

Unapokuwa Mkristo, unamruhusu Yesu kuwa Kiongozi wa maisha yako. Yeye ndiye Kiongozi wako. Unamtumikia. Anakuambia la kufanya. Unafanya kile anachotaka ufanye. Sio jukumu lako kumwambia Mungu afanye nini. Tazama 1 Wakorintho 6:19-20 na Yohana 15:1-11.

## 6. Mimi ni rafiki wa Mungu

Yeye anakupenda. Anakuita rafiki yake. Mungu anataka kuwa rafiki yako mwema. Tazama Yohana 15:12-16.

## 7. Bado ninakua (kwa hivyo tafadhali kuwa na subira nami)

Mungu alikuumba kukua. Huu ni mchakato wa maisha yote. Ni muhimu kukumbuka kuwa unahitaji kuendelea kukua kwa njia ambayo Mungu anataka ukue.
Tazama Wafilipi 1:6.

Ikiwa tunakubali kile Mungu anasema juu yetu katika Biblia, tunajua kuwa Anaona kila mmoja wetu kama watu wa kipekee sana. Mungu anakujua kwa undani. Alikuumba, na anapenda kile Alichoumba. Sasa una siku za usoni ambazo zimejaa fursa za kukufanya maisha yako kuwa ya maana na yaliyo na mafanikio kutoka kwa mtazamo wake.

Hebu tuangalie jinsi Mungu alivyotuumba. Hakuna hata mmoja wetu anayefanana na mwingine, lakini kwa njia nyingi tunafanana.

# Mimi ni nani?

**B. Niko na mwili halisi**

1. Fahamu tano
   - Kuona
   - Kusikia
   - Kunusa
   - Kuonja
   - Kugusa

2. Vichocheo vya Kimwili
   - Maji
   - Chakula
   - Hewa

**C. Niko na utu**
(vipengele vya kisaikolojia)
1. Mawazo yangu
2. Hisia zangu
3. Maamuzi yangu
4. Dhamiri yangu

**D. Niko na roho**
Mahali ambapo Mungu anaishi
Warumi 8:9



## B. Niko na mwili halisi

Kila mmoja wetu ana mwili: mikono miwili, kichwa, miguu miwili, nk. Kwa wazi, kila mmoja wetu huonekana tofauti. Lakini sisi sote tuna sehemu sawa za mwili.

Mwili wako asili unaweza kufanya vitu kadhaa.

- Unaweza kuona kwa macho yako.

- Unaweza kusikia kwa masikio yako.

- Unaweza kunusa kwa pua lako.

- Unaweza kuonja kwa ulimi wako.

- Unaweza kuhisi vitu kupitia mikono yako, miguu, na sehemu zingine za mwili wako.

Mwili huu ulio nao ni muujiza kabisa. Sehemu zote za mwili zinafanya kazi pamoja. Sayansi imechunguza sehemu tofauti za miili yetu na kugundua kuwa kila sehemu siyo ya kawaida.  Kwa kweli Mungu alifanya kazi nzuri wakati aliiumba miili yetu.

Sote tunajua mtu huhisi vipi akiwa mgonjwa. Nyakati hizo, mwili wetu wa asili huwa haufanyi kazi kwa jinsi Mungu alivyokusudia. Dhambi pia huathiri mwili wetu wa asili.

Kufanya ngono nje ya ndoa kunaweza kusababisha magonjwa ya zinaa au UKIMWI. Uvutaji sigara unaweza kusababisha saratani. Pombe inaweza kusababisha ugonjwa wa ini.

Una mwili wa asili, lakini wewe ni zaidi ya mifupa, misuli, na ngozi. Una utu. Wewe halisi umo ndani ya mwili wako asili.

## C. Niko na utu

Unaweza kuonekana kufanana sana na mtu mwingine (kwa mwili), haswa ikiwa una pacha mnayeafanana. Lakini kila mmoja wetu ni spesheli inapokuja kulinganisha jinsi tulivyo. Kuna vitu vinne muhimu vilivyo na ushawishi mkubwa juu ya utu wako. Wacha tuviangalie.

### 1. Mawazo yangu

Una ubongo-hiyo sehemu ya mwili wako. Lakini ndani ya ubongo wako kuna mawazo na kumbukumbu. Mawazo yako hukufanya uwe mtu maalum. Unachofikiria juu ya mambo kadhaa ni imani zako. Kwa mfano, “Ninaamini kuwa nyama ni nzuri kwangu, haswa minofu mikubwa ya nyama.” “Ninaamini kuna Mungu na kwamba ananipenda.”

Pia umeumba mifumo ya kufikiria katika miaka michache iliyopita. Hii inaitwa mitazamo. Una mtazamo fulani kuhusu kazi-kundi zima la mawazo na imani ambazo zina ushawishi mkubwa kuhusu jinsi unavyotenda na kuhisi unapoambiwa ufanye kazi fulani.

Somo hili la mitazamo limefunzwa kwa undani zaidi katika kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* iitwayo **Mitazamo**.

### 2. Hisia zangu

Hisia zako zina ushawishi mkubwa inapokuja kwa swala la utu wako. Jinsi (na wakati) unavyoonyesha hisia zako inaelezea mambo mengi kususu utu na tabia yako. Hakuna mtu yoyote yule anayeweza kuelewa kikamilifu jinsi unavyohisi katika hali fulani unayopitia. Lakini wanaweza kuwa na wazo nzuri, kwa sababu wao pia wana hisia zile zile ambazo unazo-hasira, furaha, huzuni, amani, hofu, nk.

### 3. Maamuzi yangu

Una nia. Unaweza kufanya maamuzi yako mwenyewe. Sehemu hii ya utu wako ni maalum kwako. Mungu aliumba kila mmoja wetu na uwezo wa kufanya uumazi. Watu wengine wanaweza kutushawishi, lakini bado tuna nguvu ya kuamua nini tutafanya. Kwa wengine wetu, hii ndio iliyotufanya kuwa na shida na polisi. Tulikataa na kutotii sheria zilizotolewa na watu wengine. Na wengine wetu walikamatwa.

Mungu anatutarajia kuwajibika kwa maamuzi tunayofanya. Hatuwezi kumlaumu mtu mwingine kwa maamuzi tunayofanya. Lazima tukabiliane na matokeo ya maamuzi yetu, hata ikiwa mambo hayatatokea kwa njia tunayotarajia.

Mungu alikupa uwezo mkubwa wa kufanya maamuzi yako mwenyewe. Una nguvu ya kuwa Mkristo aliyefanikiwa wakati unapoamua kumtii Mungu.

## 4. Dhamiri yangu

Wanyama wana uwezo wa kufikiria, kuhisi, na kufanya maamuzi. Wanyama wengine ni wenye akili sana. Lakini Mungu aliwafanya watu kuwa tofauti na wanyama wengine wote kwa kutupatia dhamiri. Hii ndio sehemu yako ambayo hukuambia wakati unafanya kitu sawa au vibaya.

Mara nyingi sisi huzungumza kuhusu dhamiri yenye hatia au dhamiri safi. Je! Wewe huhisi vibaya wakati unajua umefanya kitu kibaya? Ikiwa wewe huhisi vibaya moyoni, basi ni kwa nini huwa unahisi hivi? Kwa sababu dhamiri yako hukuambia hivyo.

Wakati Mungu aliumba watu, Aliweka dhamiri katika kila mmoja wetu kwa hivyo hatungekuwa na udhuru wowote wa kuvunja sheria za Mungu. Watu wengine wameshindwa kuwasiliana na dhamiri zao. Watu wengi ambao sio Wakristo wanakataa kusikiliza dhamiri zao.

Ikiwa una wakati mgumu kumsikiza Mungu wakati anaongea na wewe kupitia dhamiri yako, omba Mungu akusaidie uwe msikivu wa dhamiri yako. Jifunze kusikiliza dhamiri yako na kuitii mara moja. Dhamiri yako inaweza kukulinda kutokana na kushindwa na majaribu.

Ikiwa una dhamiri yenye hatia, omba na kukiri dhambi zako kwa Mungu. Atakusamehe na kuondoa hiyo hatia. Mungu atakupa dhamiri safi, iliyojaa amani.

Unahitaji kuwa mwangalifu usipuuze dhamiri yako baada ya kuwa Mkristo. Una jukumu la kumsikiliza Mungu wakati anaongea nawe

## Je, vipi kuhusu hatia ya uwongo?

Wakati mwingine Wakristo wapya huchanganya hatia ya uwongo na hatia ya kweli. Ikiwa Mkristo atatenda dhambi, mara nyingi atahisi kuwa na hatia. Hii ni hatia ya kweli kutoka kwa Mungu kupitia dhamiri yako. Ikiwa utakiri dhambi yako, Mungu ni mwaminifu na atakusamehe.

Wakristo wengi wanaendelea kishi maisha ya kuhisi hatia juu ya dhambi kwa muda mrefu baada ya kukiri kwa dhati. Katika hali kama hii, shida sio kushindwa kwa Mungu kusamehe dhambi zako. Shida ni Shetani. Yesu alimuelezea Shetani kama “mshtaki wa ndugu.” Hii ni moja ya hila za Shetani. Atafanya kila mbinu kukurejeshea kumbukumbu zako za dhambi ambazo umetubu. Atakukumbusha pia jinsi dhambi hiyo ilikuwa mbaya, na jinsi Mungu anachukia dhambi. Atakushutumu kwa kutofaulu na kujaribu kukukatisha tamaa ya kutosha ili uache kuwa Mkristo.

Tunahitaji kuwa waaminifu kabisa kwa Mungu. Huwezi kumdanganya Mungu kwa toba ya uongo. Yuko tayari kusamehe dhambi kubwa tunapokuja na kukiri kwa uaminifu kama vile Mfalme Daudi alivyofanya katika 2 Samweli 12:13.

Ikiwa Shetani ataendelea kukuletea dhambi za zamani ambazo umekiri, usijaribu kuzuia mawazo hayo. Tunahitaji kujifunza jinsi ya kufuata ushauri uliotolewa katika 2 Wakorintho 10:3-5 ambao unatuambia tulichukue mateka kila wazo na kulifanya liwe tiifu kwa Kristo. Tumia hii kama tukio la kukubaliana na Shetani kwamba ulifanya dhambi hiyo. Lakini umkumbushe kwamba Mungu amekusamehe. Kisha geuza mawazo yako kwa Mungu na umshukuru kwa msamaha wake. Tumia hii kama fursa ya kujikumbusha kuwa unataka

kumtumikia Mungu kwa moyo wako wote. Jikumbushe kuwa dhambi kila mara huwa na matokeo machungu, na unataka kuishi kila siku kwa njia ambayo itamfurahisha Mungu.

## D. Niko na roho

Unaweza kusema pia, “Mimi ni roho.” Wewe ni zaidi ya mwili ulio na utu. Wakati Mungu aliumba watu, Alituumba kwa mfani wa sura yake mwenyewe. Mungu ni roho. Amekupa roho.

Wakati mtu anapokuwa Mkristo, Mungu huja na kuishi ndani yake. Wapi? Je, Kwa ubongo wako? Hapana. Je, Kwa moyo wako? Hapana. Moyo wako unasukuma damu tu. Ni kwa hisia zako? Hapana.

Unapokuwa Mkristo, Mungu huja na anaishi katika roho yako. Roho yako iko wapi? Iko ndani yako, lakini roho sio mwili. Walakini, ni ya kweli. Hisia zako za hasira, woga, furaha, na amani ni za kweli, lakini sio za mwili. Hauwezi kumpasua mtu wazi na ukupata hasira au woga ndani. Lakini hisia hizo bado ni sehemu halisi ya kila mmoja wetu. Warumi 8:9-11 inasema kwamba Mungu anaishi katika roho yako.

Dhambi huharibu maisha. Watu ambao wanaishi katika dhambi (ambao sio Wakristo) wamekufa kiroho. Roho yao imekufa. Mungu haishi ndani yao. Lakini unapokuja kwa Kristo, na kumpa maisha yako, Yeye hutoa uhai kwa roho yako na anakuja kuishi ndani yako.

Wakati mwili wako unakufa, roho yako itaenda mbinguni na utaishi milele na Mungu-ikiwa umemruhusu Yesu akusamehe dhambi zako.

# Sura ya 2
# Hatua tano za kuwa Mkristo aliyefanikiwa

Watu wengine wana dhana kwamba ni rahisi kuwa Mkristo aliyefanikiwa. Wanafikiria kuwa ukikiri dhambi zako, Mungu ataondoa shida na matatizo yako yote na kukupa furaha, amani, na pesa. Mungu hafanyi kazi hivyo. Ikiwa unataka kuwa Mkristo aliyefanikiwa, lazima ufanye kazi na Roho Mtakatifu ili alete mabadiliko katika maisha yako.

Roho Mtakatifu atakuongoza kupitia uzoefu wako wa kila siku na kukupa fursa za kukuza nguvu za kiroho. Huwezi kukomaa kiroho kwa wiki moja au mbili. Kwa msaada wa Mungu unaweza kuendelea kukua hadi siku utakapokufa. Mungu hupima mafanikio tofauti na vile watu hupima. Leo hii unaweza kufanikiwa machoni pa Mungu ikiwa unafanya mambo ambayo anataka uyafanye. Kumbuka wewe ni mtoto wake. Kwa sababu Mungu alikuumba kwa kusudi fulani, utakuwa na furaha zaidi wakati utafuata mpango wake na kuendelea kukua.

Ikiwa una mtoto aliye na umri wa mwaka mmoja au miaka miwili, matarajio yako kwake ni kwamba atafanya mambo kama mtoto. Huwezi kukasirika kwa sababu yeye hafanyi mambo kama mtu mzima. Lakini mtoto wako akiwa na umri wa miaka 21, unatarajia tabia yake na kuzungumza kwake kuwe kwa mtu aliyekomaa. Wakati Mungu anapokuangalia, Yeye hutumia kipimo kilicho sahihi na cha haki. Anajua nguvu na udhaifu wako, na ni kiasi kipi cha ukuaji anatrajia kutoka kwako. Ikiwa unataka kuwa Mkristo aliyefanikiwa, lazima uendelee kukua.

Kwenye kurasa zifuatazo utapata hatua tano ambazo zinaweza kukusaidia kuwa Mkristo mkomavu. Tunaweza kuorodhesha hatua nyingi zaidi katika mchakato huu wa ukuaji. Lakini hizi tano ni za msingi ambazo tunahitaji kuzingatia kwa uangalifu tunapojitahidi kumpendeza Mungu

## A. Je! Hatua hizi Tano ni Zipi?

1. Kuwa Mkristo
2. Badilisha jinsi unavyofikiria
3. Weka malengo mapya
4. Jifunze jinsi ya kudhibiti hisia zako
5. Wafahamishe wengine kile Kristo amefanya katika maisha yako

Hebu tutazame kwa kina kila moja ya hatua hizi tano.

# Hatua ya 1. Kuwa Mkristo

Ni kweli kusema kuwa huwezi kuanza kuwa Mkristo "aliyefanikiwa" hadi kwanza uwe Mkristo. Biblia inauliza swali hili ili kutulazimisha kuzingatia vipaumbele vyetu maishani. "Na je, unafaidika vipi ikiwa utaupata ulimwengu wote lakini upoteze nafsi yako mwenyewe katika mchakato huu? 37 Je, kuna kitu chochote cha thamani zaidi kuliko nafsi yako?" (Marko 8:36-37 (Biblia Takatifu –SUV) Unapoangalia mambo yote ambayo ulimwengu unapeana, je, ni ya thamani sana kuliko kuishi na Mungu milele?

Ni mambo yapi yanayohusika katika mtu kuwa Mkristo? Je! Roho, akili, hisia, na nia yako zinahusika vipi katika mchakato wa mtu kuwa Mkristo?

## a. Mwache Mungu akuzungumzie kupitia Biblia

Mungu ametupatia Neno lake, Biblia, ambalo linakuambia jinsi ya kuwa Mkristo. Unaposoma Bibilia, utaweza kuona wazi ukweli ambao unaeleza jinsi mtu anaweza kuwa Mkristo. Roho Mtakatifu atazungumza nawe kupitia dhamiri yako na kukuonyesha kwa ni nini unahitaji kuwa Mkristo. Unapotoa maisha yako kwa Kristo, Yeye huja kuishi ndani ya roho yako. Yeye huleta maisha mapya ndani ya roho yako. Tazama Warumi 8:9-11.

## b. Unalielewa Neno lake kupitia akili yako

Roho Mtakatifu atakusaidia kuelewa Neno lake. Atakusaidia kuona jinsi unavyoweza kuwa Mkristo. Lazima uelewe jinsi ya kuwa Mkristo kabla ya kuwa mmoja. Haiwezekani kudanganywa ili uwe Mkristo. Akili yako lazima ihusishwe kikamilifu wakati unakuwa Mkristo.

## c. Unajibu kwa hisia zako

Unapokuwa Mkristo hisia zako zinapaswa kuhusika kikamilifu. Baadhi ya hisia unazoweza kupokea ukiwa Mkristo ni kama zifatazo:

* Huzuni-kwa sababu umemkosea Mungu. Tazama Yakobo 4:9

* Furaha-kwa sababu dhambi zako zimesamehewa na hatia imekwisha. Unaweza kuwa na furaha kwa sababu sasa wewe ni mtoto wa Mungu na una ahadi ya uzima wa milele. Tazama Luka 10:20.

* Amani-kwa sababu Yesu sasa ndiye Kiongozi wa maisha yako. Tazama Yohana 14:27.

## d. Unachagua kwa hiari yako

Lazima utende zaidi ya kufikiria juu ya kuwa Mkristo au kuwa na hisia—lazima ufanye uamuzi. Lazima uamue utafanya nini na Mungu. Je! Utakubali dhambi zako na umwombe akusamehe? Je! Utamwacha awe Kiongozi wa maisha yako? Ikiwa utajibu maswali haya kusema "ndio," basi lazima umwambie Mungu uamuzi wako. Tazama Warumi 10:9-10.

Unapomuuliza Yesu asamehe dhambi zako na kuwa Kiongozi wa maisha yako—Yeye hufanya hivyo! Yeye huja ndani ya roho yako—Na kuishi hapo! Tazama Warumi 8:9-11.

Somo hili lote la kuwa Mkristo linajadiliwa kwa undani zaidi katika *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* yaitwayo **Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?**

## Hatua ya 2. Badilisha jinsi unavyofikiria

Watu wengine wanafikiria kwamba kwa kukiri dhambi zao na kumuuliza Yesu kuwa Kiongozi wa maisha yao ndilo jambo wanalopaswa kufanya pekee ili kuwa Wakristo waliofanikiwa. Sio rahisi namna hiyo. Unapokuwa Mkristo, Mungu hubadilisha roho yako mara moja. Yeye huja na kuishi katika roho yako. Bila Mungu kuwepo katika roho yako, hiyo sehemu yako huwa imekufa.

Lakini Mungu huwa haibadilishi mara moja akili, hisia, na mapenzi yako. Lazima ushiriki kikamilifu katika kubadilisha maeneo haya ya maisha yako ikiwa unataka kuwa Mkristo aliyefanikiwa.

Mungu anasema kwamba Njia zake ni tofauti na njia zetu na mawazo yake ni tofauti na yetu (Isaya 55:8). Unahitaji kujifunza kufikiria jinsi Mungu anavyofikiria. Wafilipi 4:8 inatoa mfano wa jinsi Mungu anataka ufikirie.

**Wafilipi 4:8 (Biblia Takatifu –SUV)**

**Hatimaye, ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya heshima, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo.**

Unapozidi kujifunza Bibilia na kutumia kile unachojifunza, Roho Mtakatifu atakusaidia kuelewa jinsi Mungu anafikiria. Atakusaidia kubadilisha mitazamo yako. Warumi 12:2 ni changamoto kwetu kujifunza njia mpya ya kufikiria.

**Warumi 12:2 (Biblia Takatifu- SUV)**

**Wala msifuate kanuni za dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu**

### a. Mtazamo ni nini?

Mtazamo sio hisia. Hisia au mihemuko hazifanani na mawazo. Ubaguzi ni mtazamo. Mtazamo huhusisha kile unachofikiria kuhusu jambo fulani. Mtu anaweza kuwa na hisia kali zilizoshikamashwa katika mtazamo wa ubaguzi, kama vile hasira, chuki, au hofu.

Neno “mitazamo” linaweza kufafanuliwa kwa njia zifuatazo:

(l) Mfumo wa kufikira

(2) Tabia ya kufikiria

(3) Maoni ya kudumu

(4) Maoni ya mtu

(5) Mfumo wa kumbukumbu

Mitazamo huundwa akilini mwako na kuwa sehemu ya maisha yako hata kiasi cha wewe kutozifikiria kwa uangalifu juu yake wakati unapozitumia. Wewe huoneyesha mitazamo yako kwa jinsi unavyojibu katika shughuli zako za kila siku. Kile unachosema na kufanya na hisia unazoonyesha zinadhihirisha mitazamo yako.

Je! Wewe hufanyaje wakati dereva aliye mbele yako anakataa kusonga wakati taa ya trafiki inageuka kuwa kijani kibichi? Je! Wewe hufanyaje wakati mtu anakutukana au kukuita jina mbaya? Jinsi unavyojibu huonesha wazi mitazamo yako- mfumo wa mawazo yako kuhusu kila hali.

### b. Ninawezaje kukuza mitazamo mipya?

Mchakato wa kujenga mitazamo mipya wakati mwingine huwa ni wa polepole na wa kuvunja moyo. Unaweza kuamua kuacha kuitikia kwa haraka na hasira wakati mtu anapokukasirikia. Kwako kubadilika, huchukua zaidi ya ahadi. Mitazamo hii imekuwa sehemu ya njia yako ya kufikiria kwa miaka. Ni kwa mara chache, Mungu hubadilisha mitazamo ya mtu mara moja. Lakini kwa kawaida Yeye huwa hafanyi miujiza ya papo hapo katika eneo hili la maisha yako. Lakini unaweza kuwa na hakika kuwa Yeye yuko tayari kukusaidia kubadilisha mitazamo yako ikiwa uko tayari kufanya kazi naye

Njia moja bora ya kugundua ni mitazamo gani mipya ambayo Mungu anataka uwe nayo ni kusoma Bibilia. Tafuta jinsi Yesu alivyowatendea watu tofauti aliokutana nao na kufanya kazi nao kila siku. Tafuta haya katika Bibilia ambazo huzungumza juu ya maeneo katika maisha yako ambapo unahitaji kubadilisha njia yako ya fikra. Kitabu cha Mithali ni sehemu nzuri ya kujua jinsi Mungu anafikiria kuhusu maswala mengi tofauti unayopitia maishani. Wafilipi 2:5 inatutia moyo kukuza aina zile zile za mitazamo ambazo Yesu alikuwa nazo. Ikiwa hauna hakika kuwa mitazamo yako inampendeza Mungu, basi muulize, “Mungu, unafikiria nini juu ya hii?” Tafuta majibu Yake unaposoma Bibilia na uzungumze na Wakristo wengine.

Kusoma tu Bibilia kunaweza kuwa hakutoshi kubadilisha njia yako ya mawazo-mifumo ya mawazo yako. Kukariri Maandiko ni njia moja yenye nguvu ya kukusaidia kujenga mitazamo mipya katika mtindo wako wa maisha. Luka 6:27-38 imejaa mashauri ya kutekeleza. Unapokariri aya za Bibilia, jiambie kuwa hivi ndivyo unavyotaka kufikiria.

Kumbuka kwamba kujenga mitazamo mpya katika akili yako labda hakutafanikiwa ikiwa unategemea tu nguvu yako mwenyewe. Muulize Roho Mtakatifu akusaidie kutekeleza mitazamo hii ya Bibilia katika kila hali. Tazama Yohana 16:13. Mada ya mitazamo imejadiliwa kwa kindani sana katika *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* katika kozi iitwayo, **Mitazamo.**

## Hatua ya 3. Weka malengo mapya

Kuwa Mkristo aliyefanikiwa kunahusisha zaidi ya kuelewa Neno la Mungu. Lazima ulitumie katika maisha yako. Lazima uweke mapenzi na matakwa yako chini ya uongozi wa Mungu na ufanye mambo ambayo anataka ufanye. Biblia inasema, “Tunapaswa kupanga mipango - tukitegemea Mungu atuongoze.” (Mithali 16:9, The Living Bible) Weka malengo yako ili yawe sawa na mipango na malengo ambayo Mungu amekuwekea. Pengine unauliza, “Kwa hivyo Mungu anataka nifanye nini?”

### a. Tafuta kile Mungu anataka ufanye

Hatua ya kwanza na ya muhimu zaidi katika kuweka malengo ni kugundua mipango ya Mungu katika maisha yako ni yapi.

**Waefeso 2:10 (Biblia Takatifu –SUV)**

**Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.**

**Yeremia 29:11 (Biblia Takatifu –SUV)**

**Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za baadaye.**

Mistari hii yote miwili inadhihirisha wazi kwamba Mungu ana mipango tayari kwa kile Anachotaka ufanye. Unaweza kukubali malengo ya Mungu au kuyapuuza. Ukiyakumbatia, yatakupa nguvu ya kufanya siku zako ziwe duniani ziwe za maana. Malengo haya yanaweza kukupa mwelekeo zaidi ya mahitaji yako ya kibinafsi na matamanio maishani.

Una hatima ambayo Mungu amekuandalia maishani mwako. Haijalishi wengine wamekuambia nini — Mungu anajali maisha yako. Una kusudi la ni kwa nini upo hapa duniani. Unahitaji kugundua kusudi hilo na kuanza kufanya kile Mungu anataka ufanye.

Kwa hivyo Mungu anataka ufanye nini leo? Angalia karibu na wewe-ni mahitaji gani unayoona? Je! Unaweza kuwa sehemu ya kukidhi mahitaji hayo? Watu wengi walio karibu nawe wanahitaji tabasamu, neno la kutia moyo, sala. Hatuzungumzii tu kuhsu maamuzi makuu juu ya nani utamuoa au chaguo lako la kazi. Unapaswa kuangalia pia maswala madogo ya kila siku yanayokukumba leo.

Jifunze Biblia ili ujue jambo gani Mungu anataka ufanye. Kuna mistari mingi katika Biblia ambayo inashughulikia hali unazokabiliana nazo kila siku. Tumia kamusi ya Biblia kwenye kompyuta kupata mistari yote inayozungumza juu ya mada fulani.

Kwa mfano, utapata mistari mingi inayoonyesha kile Mungu anataka ufanye wakati unafanya kazi. Mistari mingine inashughulikia usemi wako na hisia zako, kama hasira, uchungu, furaha, na amani. Katika mistari hii ya Biblia, Mungu anakuambia jinsi anataka uishi na kuitikia kwa kila moja ya hali hizi. Usisubiri na kusema, “Kweli, nitakapoweka maisha yangu sawa mwaka ujao, nitaanza kupanga kuweka malengo kadhaa.” Anza sasa! Usisubiri hali kuwa kamilifu. Biblia inasema, “Mwenye kuuangalia upepo hatapanda.” (Mhubiri 11:4, (Biblia Takatifu – SUV) Hapa kuna aya kadhaa za Biblia ambazo zinaelezea mambo kadhaa ambayo Mungu anataka ufanye:

Marko 12:30-31

Luka 6:27-38

Warumi 13:1-5

1 Wakorintho 13:4-8

Waefeso 6:1

2 Petro 1:5-11

## b. Aina tofauti za malengo

Kuna aina nyingi tofauti za malengo ambayo Mkristo anaweza kuweka. Hapa kuna maeneo machache ambayo unaweza kuweka malengo:

1. Malengo ya kielimu
2. Malengo ya kazi
3. Malengo ya kiroho
4. Malengo ya kusoma na kukariri Biblia
5. Malengo ya tabia (maendeleo ya kibinafsi, ujasiri, uvumilivu, upendo, ukarimu)
6. Malengo ya mtazamo
7. Malengo ya kuweka maandiko katika matendo
8. Malengo ya uhusiano
9. Malengo ya kuwa na mipaka

## c. Unawezaje kuanza kuweka malengo?

Kuna aina nyingi tofauti za malengo ambayo unaweza kuweka ambayo yatakusaidia kuwa Mkristo aliyefanikiwa zaidi. Walakini, aina moja ya mpangilio wa kuweka malengo inaweza kuwa na athari kubwa katika uhusiano wako na Mungu na watu wengine. Unahitaji kujifunza jinsi ya kuweka malengo amabayo utatayatekeleza kila siku kibinafsi. Haya ni malengo madogo ambayo unaweza kuyafikia katika siku moja au mbili. Njia moja ya kuatekeleza malengo haya ya kila siku ni kuyawekea msingi wake na aya zilzizo kwenye Biblia.

Unapopata aya katika Biblia ambayo inazungumzia shida au suala unalokabiliana nalo, basi andika lengo ambalo litakusaidia kuweka katika matendo kile aya hii inakufundisha kufanya. Hapa kuna maelezo ya kina ya njia moja ya kufanya hivi.

### 1. Angalia shida katika maisha yako ya kila siku

Unaweza kuwa unakabiliwa na hali ngumu katika maisha yako leo. Unahisi kuzidiwa na mambo. Labda haujui kile ambacho Mungu anataka ufanye. Ziangalie shida hizi na ujaribu kujua ni nini kinachosababisha zitokee.

### 2. Jiulize, “Je! Mungu anajaribu kunifundisha kufanya nini leo katika eneo hili la maisha yangu?”

Omba na umuulize Mungu akusaidie kuelewa ni nini husababisha shida hii. Muulize akusaidie kuona maeneo ya maisha yako ambapo unahitaji kukua ili uweze kushinda shida hii.

### 3. Tafuta eneo moja la maisha yako ambapo unataka kukua leo

Malengo yanaweza kukusaidia kutoka katika eneo lako ambalo umezoea. Yanaweza kukuvuta zaidi ya kile unachofanya leo. Kuwa tayari kuchukua hatua. Ikiwa unapitia mpweke-weka lengo! Fanya kitu ambacho kinakuhusisha na watu wengine. Tafuta watu walio na mahitaji na uwe rafiki wao. Ikiwa una wakati mgumu kutambua maeneo ambayo unahitaji kukua, angalia orodha iliyotolewa katika 1 Wakorintho 13:4-8.

### 4. Unganisha utafiti wako wa Biblia kwa eneo hili ambalo unataka kukua

Je! Biblia inasema nini juu ya eneo hili la maisha yako? Tafuta aya hizo kwenye Biblia ambazo zitakusaidia kuelewa shida na maoni ya Mungu ya jinsi ya kuzitatua. Tafuta ahadi na ukweli ambao unaweza kutumika katika shughuli zako za kila siku.

### 5. Orodhesha vitu unavyoweza kukamilisha leo

Sasa kwa kuwa umejifunza Biblia, orodhesha malengo kadhaa ambayao utatekeleza kibinafsi. Kwanza chukua muda kufanya mawazo ya jumla ya ubunifu. Orodhesha wazo lolote ambalo lina uwezo wa kuwa lengo. Kisha chagua lengo moja la leo. Tumia miongozo iliyoorodheshwa baadaye katika sehemu hii kubuni lengo zuri la kila siku. Fanya iwe maalum kiasi kwamba wewe na wengine mwaweza kupima matokeo yake.

Baada ya hapo, weka mipango yako kwa vitendo. Tekeleza kile ulichopanga.

### 6. Tathmini matokeo

Baadaye siku hiyo hiyo au siku itakayofuata, kagua kile kilichotokea wakati ulijaribu kufikia lengo ulilolweka. Wakati mwingine hautafikia lengo lako. Lakini usikate tamaa. Jaribu tena. Usiogope kubadilisha malengo yako. Lakini kwa upande mwingine, usibadilishe lengo lako kwa sababu umeshindwa mara ya kwanza ulipojaribu.

Thomas Edison alishindwa mara nyingi kabla ya kugundua balbu nyepesi iliyofanya kazi. Kwa kweli, alishindwa zaidi ya mara 2,000 kabla ya kufanikiwa mara moja kutengeneza balbu nyepesi iliyofanya kazi. Usiwe mwepesi wa kukata tamaaa.

**2 Wakorintho 8:11 Biblia Takatifu –SUV**

**Lakini sasa timizeni kule kutenda nako, ili kama vile mlivyokuwa tayari kutamani kutenda, vivyo hivyo mkawe tayari na kutimiza, kwa kadiri ya mlivyo navyo.**

Unapoyaangalia maoni sita yaliyoorodheshwa hapo juu, angalia tena ya kwanza. “Angalia shida kwenye maisha yako ya kila siku.” Wengi wetu hatupendi migogoro. Lakini ikiwa unataka kuwa Mkristo aliyefanikiwa, basi lazima ujifunze jinsi ya kukabiliana na migogoro na kukua kupitia uzoefu huu wenye uchungu. Lazima uwe tayari kusaidia kutatua migogoro. Ni rahisi kuweka mtu mwingine chini na kufikiria, “Niko sawa, wewe ndiye umekosea.” Lakini Mungu anatafuta wanaume na wanawake ambao wanaeneza amani.

Mungu hatarajii uwe sahihi na sawa kila wakati-huo ni ukamilifu. Lakini yeye anatarajia uwe mwaminifu. Unapokosea, kubali. Kwamba Mungu bado atakupenda.

Atakusaidia kujifunza kutokana na tatizo hilo ikiwa uko tayari kuja kwake na moyo wazi na akili, tayari kujifunza. Tazama Warumi 5:3-5.

Anza kila siku na sala rahisi-Mungu unataka nifanye nini leo? Tafuta fursa za Mungu ambazo analeta katika maisha yako leo, na utafute kufanya mambo mazuri ambayo amekuumba ufanye.

### d. Alama nzuri ya kila siku ni ipi?

Kujifunza kuandika malengo mazuri ya kila siku mara nyingi ni kugumu pale mwanzoni. Wengi wetu hatujawahi kufanya hivi hapo awali. Kila jambo jipya huwa kamilifu kupitia mazoezi. Kadri unavyoandika malengo, ndivyo utakavyozidi kuwa bora, na kadri yatakavyokusaidia katika ukuaji wako kama Mkristo. Hapa kuna miongozo michache ambayo itakusaidia kujifunza jinsi ya kuboresha malengo yako ya kila siku.

1. **Ni rahisi.** Lengo linasema jambo moja. Halina shaka akilini mwako kuhusu kile unachotaka kukamilisha.

2. **Ni maalum.** Lengo linasema wazi kile unachotaka. Mara nyingi malengo yetu ni ya jumla sana. Wacha tuangalie lengo hili, “Nitakaribia Mungu.” Lengo hili ni kubwa sana. Utakuaje karibu na Mungu? Itakuwa busara kuamua juu ya jambo moja ambalo unaweza kufanya ambalo hakika litakuvuta karibu na Mungu. Liweke hilo kama lengo lako la kwanza. Unapolitimiza, weka lengo lingine ambalo litaimarisha lile lengo la kwanza na pia kukusadia kuchukua hatua moja zaidi katika uhusiano wako na Mungu. Daima kuwa wazi na aliye na lengo maalum katika utumizi wa maneno ya kila lengo. Weka iwe rahisi kwa kuandika kitendo kiomoja tu.

3. **Ni la maana.** Lengo lako linahusiana na maisha yako leo. Lengo, liseamlo “Ikiwa nitapata utajiri, nitatoa shilingi 5000 kwa kanisa langu kila Jumapili,” halina maana sana hadi pale utakapotajirika. Unapopata utajiri, basi weka malengo yanayolingana na utajiri wako. Kusudi lako lazima litokane na kile unachojua kinawezekana katika maisha yako leo. Pia, lazima lilete mabadiliko ambayo unatka yafanyike.

4. **Inatekelezeka.** Je! Unaweza kukamilisha lengo hili leo? Lengo kama vile kusema, “ninapojaribiwa, nitatambua kwamba ni Shetani ananijaribu,” inasikika nzuri, lakini je, inatekelezeka? Utakumbukaje kujiambia kuwa jaribu limetoka kwa Shetani “kila wakati unapojaribiwa”? Lengo hili linaonekana kuwa la kiroho, lakini linaweza kuwa jaribio kubwa sana la kwanza kwa Mkristo mpya kuweza kulishinda.

   Anza kwa malengo rahisi, mafupi ambayo una uhakika unaweza kuyatekeleza kwa siku moja. Chukua lengo hili kama mfano, “Leo nitaweka orodha ya kila wakati ninapojaribiwa kutenda dhambi.” Unaweza kufanya lengo hili kuwa maalum zaidi kwa kuorodhesha aina moja tu ya jaribu, kwa mfano, “Leo nitafanya orodha ya kila wakati ninapojaribiwa kulaani.”

5. **Inaweza kupimwa.** Je! Ungeweza kupima vipi lengo hili? “Leo nitakaribia Mungu.” Lengo hili halijaandikwa kwa njia ya kulifanya iwe rahisi kulipima. Ikiwa unataka kuhakikisha kuwa unafanya maendeleo, unahitaji kuandika lengo lako kwa njia ambayo unaweza kupima kwa urahisi maendeleo yako. Lengo linaweza kupimwa: “Leo nitafanya orodha ya kila wakati ninapojaribiwa kutenda dhambi.” Unapoandaa orodha, unakamilisha shughuli ambayo inaweza kupimwa.

Ni vigumu kuandika malengo ambayo yanaweza kupimwa kwa urahisi. Lakini ni muhimu ikiwa unataka kuhakikisha kuwa unaendelea. Hapa kuna maswali manne ambayo unaweza kujiuliza unapoandika lengo lako:

Ni nini kitakachopimwa?

Nitatumia zana gani kuipima?

Je! Ni rahisi kupima?

Mtu mwingine anawezaje kupima maendeleo yangu?

Malengo haya ni ya vitendo na yanayoweza kupimika. “Usiku wa leo nitaandika majaribu matatu niliyoyapata leo.” “Nitamwuliza Beth anisamehe kwa kumkasirikia jana.”

6. **Ina manufaa kwangu.** Kusudi nzima la kuweka malengo ya kibinafsi ya kutekeleza ni ili kukusaidia kukaribia Mungu. Fikiria mbele. Unapoandika lengo lako, jiulize, “Je! Lengo hili litanisaidiaje kukua?” Unapojibidiisha kukamilisha kila lengo, je, unaweza kuona jinsi inakusaidia kuwa Mkristo bora?

Miongozo hii sita siyo hakika ya wewe kufanikiwa. Kuandika malengo mazuri ya maombi ya kibinafsi hakufkuanyi kuwa Mkristo aliyefanikiwa. Kwa kweli, malengo ni zana tu-kitu cha kukusaidia kukua. Mungu anajali sana ukuaji, sio “Je! Uliandika malengo mazuri?” Hata hivyo, ikiwa utajifunza jinsi ya kuandika malengo mazuri, na uwe mwaminifu kuyatimiza malengo haya, Mungu atakusaidia kukua yule mtu ambaye anataka uwe. Mungu hatarajii ukamilifu kutoka kwako, lakini anatarajia uweke katika matendo mafundisho yake maishani mwako.

Unapoangalia siku za usoni, unaona nini? Je! Unataka kuwa mtu wa aina gani kutoka sasa? .. miaka mitano kuanzia sasa? .. miaka kumi kutoka sasa? Mungu humpa thawabu Mkristo anayejitolea kuwa mwaminifu kwake. Je! Unaweza kujiona miaka kumi kutoka sasa kama mtu ambaye ameishi kwa uaminifu kwa Kristo? Je! Unajioana kama mtu aliyeamua kutii sheria na mafunzo ya Biblia kama jambo la kipaumbele?

Changamoto nyingine inayokukabili kwa maisha yako yote ni kukuza udhabiti maishani. Je! Wewe ni mtu ambaye yuko tayari kupambaana na “Goliathi” leo, lakini unaogopa kivuli chako mwenyewe kesho? Je! Uko juu ya ulimwengu siku moja na katika bonde la msongo wa mawazo na kuvunjika moyo siku inayofuata? Mungu anaweza kukusaidia kujenga udhabiti maishani mwako. Utaendelea kuwa na siku nzuri na siku mbaya. Lakini kupitia hayo yote, unaweza kujifunza jinsi ya kumwamini Yesu na sio kuzidiwa na shida zinazokuja maishani mwako. Hakuna tiba ya kimiujiza inayosubiri mtu anayehitaji udhabiti maishani. Inachukua kufanya kazi kwa bidii na kuweka macho yako kwa Yesu na mafundisho yake.

## Hatua ya 4. Jifunze jinsi ya kudhibiti hisia zako

Wewe sio Mkristo kwa sababu tu “unahisi umeokoka,” haijalishi unajihisi vipi. Hata hivyo, hisia zako ni sehemu muhimu sana ya maisha yako ya kila siku. Mungu alikupa hizi hisia. Sasa lazima ujifunze jinsi ya kutumia hisia zako kwa njia ya kufanya maisha yako yawe ya kumfurahisha na ya kumpendeza kwa Mungu. Katika Biblia Mungu ana mengi ya

kusema kuhusu hisia tofauti tulizo nazo kama binadamu. Unahitaji kugundua jinsi hisia zako zinaweza kukusaidia kuwa Mkristo aliyefanikiwa hata zaidi.

Moja ya hatua za msingi za ukuaji katika eneo hili la maisha yako ni kuzijua hisia zako. Jifunze kutambua jinsi na wakati unapotumia hisia tofauti. Zikubali, na ujifunze kuzitumia. Usiruhusu hisia zako kutawala maisha yako yote. Jinsi unavyojihisi haipaswi kuwa jambo kuu inayotawala maamuzi unayofanya.

Watu wengine wana tabia ya kutawaliwa na "hsia ya ghafla." Wao huwa wepesi wa kudhihirshia hisia zao kwa haraka. Kwa Siku moja (au dakika chache) wanaweza kuonekana walio na msisimko na furaha. Siku inayofuata (au dakika chache baadaye) wanaweza kuonekana tena kuzama katika vilindi vya kukata tamaa, au kuishi katika ulimwengu wao pekee ambao umegubikwa na giza. Watu wengine nao huishi katika "friji ya hisia." Wao huwa hawaoneshi hisia zao wazi wazi. Ugumu wa mioyo yao huwa hauoneshi hisia ya kusisimuka.

Mungu anataka uhisi furaha ya kuishi naye. Anaweza kukusaidia kupata njia za ubunifu za kuelezea hisia zako. Unaweza kupokea furaha ya wokovu wake. Unaweza pia kusoma Agano Jipya kuona jinsi Yesu alivyoonyesha hisia tofauti. Mungu anataka ukue ili uweze kudhibiti hisia zako na uwaeleze mambo kwa njia ambayo watu wanaweza kuona kuwa Yeye ndiye Kiongozi wa maisha yako.

Kudhibiti hisia zako haimaanishi kuzishikilia kwa ndani. Labda itakuwa bora kusema unahitaji kujifunza jinsi ya kudhibiti hisia zako. Mungu anataka uwe mtu aliye na hisia kama binadamu yeyote yule. Jambo muhimu ni kujifunza kuelez kwa njia ambazo huleta utukufu kwa Mungu.

### a. Unajifunza kudhibiti hisia zako kwa kukuza mitazamo yenye msingi wa Maandiko

Katika hatua ya Pili iitwayo, "Badilisha jinsi unavyofikiria," tulijadili tofauti kati ya mitazamo na hisia (hisia). Mtazamo ambao unayo kwa mtu au hali fulani ndiyo huamua jinsi takavyoitikia kupitia hisia zako. Katika hali nyingi, hisia zako ni matokeo ya mtazamo wako katika hali fulani.

Ikiwa unataka kubadilisha jinsi unavyoonyesha hisia zako, ni lazima kwanza ukuze mitazamo mipya kulingana na mafundisho ya Biblia. Marko 3:1-8 inazungumzia kuhusu wakati Yesu alikasirika. Je! Ni mawazo yapi yalikuwa yakipitia akilini mwa Yesu wakati alipokuwa akihisi kukasirika? Alionyeshaje hasira yake? Majibu ya maswali haya yatafunua mitazamo yake kwa hali hiyo.

### b. Unapokuwa na "hisia zisizo sawa," zipeane kwa Mungu kupitia sala

Hisia za mtu huwa siyo nzuri wala mbaya. "Ni za kadri." Mungu alituumba na uwezo wa kuonyesha hisia mbali mbali. Kwa hivyo ni nini "hisia mbaya?" Wakati hisia zozote zinaonyeshwa kwa wakati usiofaa au kwa njia mbaya, ni "hisia mbaya." Kwa mfano, mwenzake Bill amesikia tu kutoka nyumbani kwamba wazazi wake wameuawa. Ikiwa Bill atatoka akicheka, huo ni wakati usiofaa na mahali pa kuelezea hisia za furaha.

Unapaswa kufanya nini wakati unahisi kuonyesha hisia yako katika wakati usiofaa? Usifanye tabia ya kuikandamiza au kuishikilia ndani. Jifunze jinsi ya kuachilia hisia hizi kwa Mungu kupitia maombi. Mwambie Mungu haswa jinsi unavyohisi. Unapomwambia jinsi unavyohisi, hii inaweza kuondoa kwa muda hisia hii ndani yako.

Suluhisho za kudumu au za muda mrefu za “hisia mbaya” zina asili yake katika mitazamo yako. Unahitaji kubadilisha mtazamo ulio nao dhidi ya mtu au kitu fulani ambacho kilisababisha ujibu kwa “hisia mbaya.”

Sote hupitia kwa hisia kama chuki, hasira, au hofu kwa nyakati tofauti katika maisha yetu. Labda mtindo wako wa zamani wa kujibu ulikuwa kuruhusu hisia hizi kudhibiti mawazo, maneno, na vitendo yako. Lakini kwa kuwa sasa umekuwa Mkristo, unaweza kubadilisha na kukuza mifumo mingine mipya ya kujibu. “Lakini nifanye nini wakati hisia hizi mbaya'zinapokuja?” Kwa msaada wa Mungu, unaweza kumruhusu achukue hisia hizi na badala yake akupe hisia zinazofaa zaidi kwa hali hiyo. Kwa mfano, mara nyingi tunaposhikwa na hasira, Mungu huenda angependa tuitikie kwa huzuni.

Kusudi lako la mwisho linapaswa kuwa kujibu kwa hisia ambayo Mungu anataka ujibu nayo. Kusudi lingine ni kujifunza kuhisi jinsi Mungu anahisi katika kila hali. Unapojifunza Biblia na kuomba, Mungu atakusaidia kujifunza jinsi Anahisi juu ya vitu unavyokabili maishani. Atakupa nguvu ya kujibu vivyo hivyo

Biblia inafundisha kwamba unapaswa kuwa mkuu wa hisia zako. Usiruhusu watu au shida kudhibiti hisia zako.

Inachukua muda kujifunza jinsi ya kusimamia hisia zako kwa njia ambayo Mungu anataka. Kama Mkristo anayekua, usiruhusu hisia hasi au ukosefu wa hisia za kiroho kukukasirisha. Baadhi ya hisia muhimu sana ambazo zinapaswa kuwa katika maisha ya Wakristo ni upendo, amani, na furaha. Hisia hizi tatu zinaweza kuwa hazipo kila wakati ndani yako, lakini zinapaswa kuzidi kuwa na nguvu kila siku katika maisha yako.

### c. Jifunze kujwa msikivu kwa hisia za watu wengine

Ni rahisi kuwa mbinafsi na kujifikiria tu wewe mwenyewe. Lakini Yesu anataka tuwafikirie wengine na kujali hisia zao. Biblia inasema, “Jinsi yule mtu mwingine anavyohisi ni muhimu. Hatuko huru kufanya mambo yatakayowaletea wengine machungu”
(1 Wakorintho 10:29, Biblia Maisha Mapya)

Jiulize swali hili, “Je! Mungu ana hisia zipi kunihusu, na kwa watu wengine ambao ninakutana nao kila siku?” Jaribu kujali hisia za Mungu. Biblia inasema wazi kuwa Mungu yuko tayari kutusamehe tunaposhindwa. Lazima tujifunze kuishi kwa mtazamo wa “kutubu muda baada ya muda.” Unaweza kujaribiwa kwa kuwakasirikia watu wengine wanapokukosea. Kwa hivyo kuwa tayari kuwasamehe na usiweke kisasi dhidi yao.

Lazima pia uwe tayari kukubali msamaha wa Mungu unaposhindwa. Usiruhusu hisia za kukata tamaa kukuzuia kumkubali Mungu baada ya kushindwa. Mungu atakusaidia kukua, hata ikiwa unahisi kama mtu aliyeshindwa. Ahadi ya Mungu kwako ni ya kweli, “Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.” (Wafilipi 4:13 Biblia Takatifu–SUV) Mungu atakupa nguvu ya kihisia unayohitaji kukabiliana na kila changamoto leo. Anaweza pia kukupa nguvu na moyo wa kujali jinsi mtu mwingine anavyohisi kuhusu hali hii.

## Hatua ya 5. Wafahamishe wengine kile Kristo amefanya katika maisha yako

Ni muhimu sana kuchukua hatua nne za kwanza za kuwa Mkristo aliyefanikiwa. Unapozifanyia kazi hatua hizi nne, unaweza kuwafahamisha wengine kile Kristo anachofanya katika maisha yako.

Ikiwa unaishi maisha ya Kikristo yenye mafanikio, wengine watataka kujua jinsi unavyofanya. Hii ni fursa nzuri kwako kuwaelekeza kwa yule ambaye kweli ameleta mabadiliko hayo, Roho Mtakatifu. Moja ya malengo yako mapya inapaswa kuwa kuwafahamisha wengine kile Yesu anafanya katika maisha yako. Ni ipi njia bora ya kufanya hivyo?

### a. Toa upendo wako kwanza

WaKorintho wa Kwanza 13:1-8 inatuambia jinsi upendo wa kweli ni muhimu na jinsi tunaweza kuonyesha upendo huu kwa wengine. Hizi ni njia rahisi za kutekeleza za kuonesha na kushiriki upendo wako na wengine. (Walakini, sio rahisi!) Upendo ni moja ya nguvu kubwa katika ulimwengu wetu. Upendo wako, zaidi ya kitu kingine chochote, utamshawishi mtu mwingine kwamba, kuwa Mkristo ni jambo nzuri.

### b. Tafuta wale ambao wana mahitaji halisi

Mara nyingi watu huwa wako tayari kupokea maoni mapya hivi kwamba wanapokuwa na shida, kupata suluhu peke yao huwa ni vigumu. Katika hali hii, mara nyingi watapendezwa kusikia jinsi Yesu Kristo anaweza kuwasaidia kwa shida zao. Uliza Roho Mtakatifu akuelekeze kwa watu ambao wana mahitaji.

### c. Tafuta wale wanaotaka msaada

Kuna watu wengi ambao wana mahitaji halisi. Walakini, sio wote wanaotaka msaada. Usilazimishe watu kukusikiliza. Ikiwa hawataki msaada, basi hakuna kubwa unaloweza kuwafanyia isipokuwa kuendelea kuonyesha upendo kwao. Acha Roho Mtakatifu afanye kazi nao katika kubadili mitazamo yao. Kuwa tayari kuwasaidia kila wanapokuja kwako kwa msaada. Ni muhimu sana kuonyesha upendo wako kwa watu kama hawa ili waweze kuona kwamba Yesu hubadilisha maisha ya mtu.

### d. Usihubiri au kubishana

Unapowashiriksisha watu wengine kwa kile Kristo amefanya katika maisha yako, usimhubilie. Usije na mtazamo usemao, “Mimi ni bora kuliko wewe.” Na usiwaambie watu shida walio nayo au kwamba wako njiani kwenda kuzimu. Toa ujumbe chanya. Shiriki kile Mungu amefanya katika maisha yako. Acha Roho Mtakatifu awahukumu kuhusu dhambi zao.

# B. Jinsi ya kuanza kutumia hatua hizi tano

Sasa kwa kuwa una ufahamu wa kimsingi wa hatua hizi tano za kuwa Mkristo aliyefanikiwa, ni wakati wa kuchukua hatua. Kujua tu hatua tano hakutakubadilisha.

Mungu alikuumba kwa kusudi-kwamba ufanye kazi nzuri alizopanga uzifanye. Tazama Waefeso 2:10. Mpango wa Mungu kwako umejaa mafanikio-kutoka kwa mtazamo wake. Njia aliyonayo kwako imejaa uhuru na kusudi.

Lakini shetani pia ana mpango usiyo mwema kwako. Kila hatua unayochukua kuelekea kwa Mungu inamfanya shetani kuwa kichaa. Atafanya kila awezalo kukukatisha tamaa, kukudanganya, na kuvunja moyo. Shetani hataki ufurahie mafanikio ambayo Mungu anayo kwa ajili yako. Shetani anataka ukae katika utumwa wa dhambi.

Kwa hivyo unalo chaguo-kuweka mawazo yako katika kufuata njia ambayo Mungu amekutengea kama yako- njia ya mafanikio ya kweli. Au unaweza kufuata fursa ambazo shetani huweka mbele yako na ujikute katika utumwa mkubwa zaidi.

Maoni yafuatayo yameundwa kukusaidia kuanza kuweka katika matendo hatua tano za kuwa Mkristo aliyefanikiwa. Moja ya mikakati muhimu ya kukusaidia kwa hatua hizi tano za kufanikiwa ni kutafuta njia bora za kuchukua mafundisho ya Biblia na kuyaweka kwa vitendo katika maisha yako ya kila siku. Unahitaji kuomba Mungu akusaidie kwa hii kila siku.

## 1. Chagua sehemu ya Maandiko yenye maana

Sehemu ya maandiko yenye maana ni moja ambayo inahusiana moja kwa moja na swali, shida, au shauku ulio nayo.

## 2. Chukua muda kukariri maandiko

Jiwekee malengo kadhaa juu ya aya ngapi utakazokariri kila wiki au mwezi.
Jaribu kutumia muda wa ziada kwenye kumbukumbu ya Jumapili. Tazama Isaya 58:13-14.

## 3. Tumia wakati kutafakari juu ya Neno la Mungu

Kutafakari kuna msingi wake katika wazo la kuangalia maisha kupitia mtazamo wa Mungu. Je! Mungu anafikiria nini juu ya hili? Mungu anahisi vipi kuhusu hili?
Unaweza kutumia wakati wako kusoma Neno la Mungu kabla ya kulala, kwa sababu mawazo yako ya mwisho jioni yanabaki akilini mwako usiku kucha na kusaidia kuweka mitazamo yako kwa siku inayofuata. Tazama Zaburi 63:5-6.

## 4. Fikiria kuhusu Neno la Mungu wakati unapofanya vitu ambavyo havihitaji umakini wako wote

Kitabu cha Kumbukumbu ya Torati 6:7 kinaorodhesha mara nne mchana ambapo tunaweza kufikiria na kuzungumza juu ya Neno la Mungu:

a) Unapokuwa nyumbani (kwa mfano, wakati wa kula, au wakati wa kupumzika au kufanya kazi).

b) Unapoenda nje kutembea (au unaposafiri kwa kutumia gari au gari moshi).

c) Unapoenda kulala.

d) Jambo la kwanza asubuhi.

## 5. Pata msaada wa rafiki mmoja au wawili

Ni rahisi kukata tamaa kwa aina hii ya zoezi ikiwa unafanya yote haya peke yako.

Lakini ikiwa una mtu wa kuongea naye, hii itakutia moyo kuitekeleza.
Weka malengo kwa pamoja na rafiki na uangalie kuwa kila mmoja wenu unayatimiza.

Hapa kuna maandiko kadhaa ambayo yatakusaidia kujifunza mawazo, malengo na hisia za Mungu:

Mathayo 5-7
Wakolosai 3
Yohana 15
1 Wathesalonike 4
1 Wakorintho 13
Waebrania 12
Warumi 6-8
Yakobo 1
Wagalatia 5

Ukuaji unaoupokea kama Mkristo huleta kuridhika halisi kwa moyo wako. Mafanikio ya kweli machoni pa Mungu huleta amani ya kweli ndani, haijalishi jinsi maisha yanaweza kuwa mabaya na kwa kiasi kipi. Katika sura hii tulizungumza juu ya mambo ambayo unaweza kufanya ili kuweze kukua kiroho, kiakili, na kihisia. Yakobo 1:2-4 na Warumi 5:3-5 zinatuhimiza kukubali majaribu magumu wakati yanapokuja kwa sababu Mungu atayatumia kukuza tabia njema na nguvu ndani yetu.

**Warumi 5:3-5 (Biblia Takatifu –SUV)**

**Wala si hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta subira; 4 na kazi ya subira ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; 5 na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.**

Pamoja na ukuaji huu wote, lazima ufanye kazi ya kukuza uadilifu na imani za ndani. Kuwa Mkristo aliyefanikiwa haimaanishi kuwa unatii kwa uangalifu sheria 650 za Mungu kila siku. Mafanikio ya kweli yanamaanisha kubadilika ndani ili kutii sheria za Mungu kwa sababu unataka. Maadili yako ya kibinafsi yanahitaji kuwa kama yale Yesu alikuwa nayo.

Haiwezekani uwe mtu ambaye Mungu anataka uwe kwa kupitia juhudi na kazi yako mwenyewe. Hata ujitahidi namna gani, hautatimiza kile kile Mungu anataka. Ndiyo sababu ametoa Roho Mtakatifu kuwa Mwalimu wako, Kiongozi, Mwongozo, na Msaidizi. Kwa msaada wake unaweza kukabili kila siku kwa ujasiri. Atakupa nguvu ya kukabiliana na kila changamoto unayokumbana nayo, ukiwa unaendelea kumwamini.

Unaposhindwa, uwe tayari kukiri. Usijidanganye kwa kuamini kuwa Wakristo waliokomaa hawafanyi dhambi. Wao hufanya. Alama halisi ya ukomavu inaonyeshwa na jinsi unakabiliana na kufeli kwako. Unakiri makosa yako hata ikiwa hakuna mtu mwingine anayeona kutofaulu kwako au dhambi yako. Unakiri kwa sababu ya imani yako ya ndani, sio kwa sababu ya shinikizo la nje. Ukomavu wa kweli unaonyeshwa katika maisha yako unapompa Roho Mtakatifu sifa kwa kile anachofanya katika maisha yako.

# Sura ya 3
# Roho Mtakatifu

Katika kozi hii tumezungumza mengi juu ya Roho Mtakatifu na sehemu yake katika kutusaidia kuwa Wakristo waliofanikiwa. Unamjuaje vyema Roho Mtakatifu? Je! Yeye ni kivuli tu cha roho katika akili yako? Kwa kiwango cha moja hadi kumi, utajipa alama ngapi ya jinsi unavyomjua Roho Mtakatifu? Wacha tuangalie kwa undani yeye ni nani na anafanya nini katika maisha yetu.

## A. Roho Mtakatifu ni nani?

Biblia ndio mahali pazuri pa kugundua Roho Mtakatifu ni nani. Kuna mambo machce mno kuhusu yanayosemwa kuhusu Roho Mtakatifu katika Agano la Kale. Walakini, Agano Jipya lina marejeleo mengi juu ya Roho Mtakatifu. Kwanza, wacha tufafanue maoni kadhaa mabaya juu ya ni nani Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu sio Yesu Kristo. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba baada ya kifo na ufufuo wake atarudi mbinguni. Lakini wafuasi wake hawangeachwa peke yao. Yesu alisema Roho Mtakatifu atakuja kuwasaidia. Yesu hakuwahi kusema Yeye mwenyewe alikuwa Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu sio jina lingine la Mungu Baba. Yesu hakuwahi kumuelezea Baba yake wa mbinguni kama Roho Mtakatifu. Waandishi wa Agano Jipya hawasemi kamwe kwamba Roho Mtakatifu ni mtu yule yule kama Mungu Baba. Walakini, Biblia inaonyesha wazi kwamba Roho Mtakatifu anahusishwa sana na Mungu Baba na Yesu Kristo.

### 1. Roho Mtakatifu ni Mtu

Kitabu cha Yohana kinatupa habari za kina kuhusu kile Yesu aliwaambia wanafunzi wake juu ya Roho Mtakatifu. Katika sura ya 13 - 16, Yesu anataja Roho Mtakatifu kama mtu halisi. Katika Yohana 16:7-11, Yesu anafafanua mambo kadhaa ambayo Roho Mtakatifu atafanya katika ulimwengu wetu.

Roho Mtakatifu si roho ya kuelea ulimwenguni kote. Yeye ni mtu wa kweli, na hawapaswi kuitwa “kitu.” Waefeso 4:29-32 anasema kwamba Roho Mtakatifu ana hisia-tunaweza kumhuzunisha Roho Mtakatifu. Yeye pia ana akili na upendo. Tazama Warumi 8:27 na 1 Wakorintho 12:11.

### 2. Roho Mtakatifu ni Mungu

Moja ya sifa ambazo huweka Mungu mbali na viumbe vyote vilivyoumbwa ni kwamba yeye yuko kila mahali. Yeye yuko kila mahali kwa wakati mmoja. Biblia inafundisha wazi

kuwa ikiwa Roho Mtakatifu wa Mungu haishi ndani yako basi wewe sio Mkristo. Tazama Warumi 8:9. Njia ya pekee ambayo Roho Mtakatifu anaweza kuishi katika maisha ya mamilioni ya Wakristo wakati wote huo ni ikiwa Ana uwezo wa kuwapo kila mahali kwa wakati mmoja.

Unaposoma Agano Jipya, unatambua kwamba waandishi wa Biblia wanasema kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu, si malaika au mtu mwingine aliyeumbwa. Kwa mfano, Petro anasema kwamba Roho Mtakatifu ndiye aliyewaongoza wanaume ambao waliandika vitabu vya Biblia. Tazama 2 Petro 1:20-21.

### 3. Roho Mtakatifu ni sawa na Mungu Baba na Yesu

Yesu wala mwandishi yeyote yule wa vitabu vya Biblia hawajamuweka Roho Mtakatifu katika nafasi ya chini kuliko Mungu Baba. Kama tutakavyoona katika kitabu hiki chote, Roho Mtakatifu na Mungu Baba na Yesu kila mmoja ana maeneo yake tofauti ya huduma kama Mungu. Kiwango cha usawa wao kinaonyeshwa wakati waandishi wa maandiko wanapozungumza kuhusu Roho Mtakatifu. Kwa kweli yeye ni Mungu na Mungu kamili. Yeye sio “naibu rais” au mtu wa nambari ya 3. Anashiriki ukuu na Mungu Baba na Mungu Mwana. Wakristo wengi huuita huu utatu wa Mungu.. Watu hawa watatu ni Mungu—Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Wao sio Mungu watatu tofauti.

## B. Je! Roho Mtakatifu hufanya nini katika maisha yako unapokuwa Mkristo?

Hata kabla ya watu kuwa Wakristo, Roho Mtakatifu hutilia maanani sana maisha yao. Mungu huwapenda wenye dhambi kabla hata hawajaitikia upendo wake.

### 1. Anakuhukumu dhidi ya dhambi

Wakati ulikuwa mtoto mchanga tu, Roho Mtakatifu alianza kukufanya ujue dhambi. Yohana 16:6-11 inasema kwamba Roho Mtakatifu yuko kazini katika ulimwengu wote, akiwahukumu watu kwa dhambi zao na kuwaonyesha kuna njia bora ya kuishi. Roho Mtakatifu huongea na watu kupitia kwa dhamiri zao. Ikiwa watu wataendelea kufanya bidii kupuuza dhamiri zao, basi kuna uwezekano wao kufikia mahali ambapo hawasikii tena Roho Mtakatifu wakati Anawatia hatiani kupitia dhamiri zao.

Katika matukio kadhaa, Roho Mtakatifu atachukua hatua kali kupata usikivu wa mwenye dhambi. Matendo sura ya 9 inaelezea jinsi Sauli alivyopofushwa macho na kusikia sauti ya Mungu ikiongea naye. Tunahitaji kuwa waangalifu ili tumsikilize Roho Mtakatifu. Hatuna uhakika kwamba Mungu atatumia hatua kali kuongea na sisi. Athari kubwa zinatusubiri Ikiwa tunajua ukweli, na kuchagua kuupuuza.

Mtu ambaye sio Mkristo amefafanuliwa katika Biblia kuwa mtu “ambaye ni kipofu wa kiroho.” Watenda dhambi mara nyingi huwa hawaelewi athari mbaya za dhambi zao. Shetani amewahadaa kuamini kuwa njia yao ya kuishi ni sawa. Roho Mtakatifu huja na kumwambia kila mwenye dhambi, “Una utupu ndani ya moyo wako. Hauwezi kukidhi mahitaji yako kikamilifu. Ni Mungu tu anayeweza kujaza utupu huo moyoni mwako”. Inaweza kuwa rahisi kwako kukumbuka hisia za kujihisi utupu ulizokuwa nazo kabla ya kuwa Mkristo.

Usifanye makosa, Roho Mtakatifu anawatia hatiani watu wote kuhusu dhambi, sio watu wabaya tu. Warumi 3:23 inasema watu wote wametenda dhambi. Ikiwa “haujisikii Roho Mtakatifu akikuhukumu kuhusu dhambi yoyote,” basi haumsikii. Ikiwa una wakati mgumu kujua ni dhambi gani unazofanya, basi omba na umuulize Roho Mtakatifu azungumze nawe kwa wazi ili ujue wakati unatenda dhambi.

Lakini wakati huo huo, usimdai Mungu kuzungumza nawe wakati unajua umevunja moja ya sheria za Mungu. Kwa mfano, ikiwa unaiba pesa (hakuna mtu anayeiba pesa za mtu kwa bahati mbaya), unajua hiyo inavunja moja ya sheria za Mungu. Usifanye udhuru na kusema, “Ni sawa kwangu kuiba, kwa sababu sikusikia Mungu akizungumza nami na kusema ilikuwa mbaya.” Tayari amezungumza katika Biblia. Unapojua ukweli, una jukumu la kuitii.

Kama vile Roho Mtakatifu anadhihirisha hali asili ya dhambi na matokeo yake mabaya, Yeye pia humfunulia mwanadamu maisha mbadala ya Kristo. Mungu atakusamehe ukikubali dhambi zako, na kuzikiri.

## 2. Anakuvuta kwa Kristo

Roho Mtakatifu huvuta watu kwa Mungu. Wenye dhambi hawatafuti Mungu, Mungu ndiye huwatafuta wenye dhambi. Hata kabla ya wewe kugeuka na kuachana na dhabi zako kisha umkubali, Mungu bado anakupenda na kila mtu mwingine yeyote aliye katika ulimwengu huu.

Roho Mtakatifu hukuongoza kwenye ukweli halisi wa maisha. Yohana 16:13 inasema kwamba Roho Mtakatifu hutuongoza katika kweli yote, sio sehemu tu ya ukweli. Zingatia neno “mwongozo.” Linazungumzia juu ya mchakato. Roho Mtakatifu hatakupa ukweli wake wote. Yeye anataka uone ukweli wake, sio tu kujaza kichwa chako kwa ukweli wa Biblia.

## 3. Yeye huja na kuishi katika roho yako

Wakati mtu anaamua kutoa maisha yake kwa Mungu, na kuanza kumfuata, Roho Mtakatifu huja na kuishi ndani yake. Warumi 8:9 inaweka wazi kuwa haya ni mabadiliko ya papo hapo. Mara tu unapokuwa Mkristo, Roho Mtakatifu huja katika maisha yako. Yeye hasubiri siku, wiki, au mwezi kabla ya Yeye kuja katika maisha yako. Roho Mtakatifu anataka kukusaidia kuendesha maisha yako, zaidi ya kukuhukumu kwaajili ya dhambi zako. Yeye anataka kukusaidia kukua kiroho na kuwa Mkristo mkomavu.

Wakati wa wokovu, mtu hupokea maisha mapya ndani ya moyo wake. Roho Mtakatifu huleta maisha haya mapya kwako.

**Warumi 8:11 Biblia Takatifu –SUV**

**Lakini, ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na mili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.**

Roho Mtakatifu haingii ndani yako kisha akakaa kimya kona ya maisha yako wakati unaendelea kufanya kile unachotaka kufanya siku baada ya siku. Yeye anataka kuwa na sehemu ya kuendesha maisha yako. Mojawapo ya mambo ya kwanza ambayo Roho Mtakatifu anataka kufanya ni kukujulisha kuwa wewe kwa kweli ni Mkristo. Biblia inasema, “Kwa Roho yake Mtakatifu huongea nasi ndani ya mioyo yetu, na anatuambia kuwa sisi ni watoto wa Mungu.” (Warumi 8:16, Tafsiri Mpya)

Usishangae ikiwa mashaka yatajaa katika akili yako. “Labda mimi sio Mkristo. Ninawezaje kuwa na hakika hii itafanya kazi maishani mwangu? Simsikii Mungu akinizungumzia. Sisikii tofauti yoyote.” Mawazo haya na mengine yanaweza kutiririka akilini mwako na kujaribu kuiba ujasiri ambao Mungu anataka kukupa. Utalazimika kuamini kile Biblia inasema. Ikiwa umekiri dhambi zako kwa dhati na kumuuliza Yesu kuwa Kiongozi wa maisha yako, basi ukubali huu kama ukweli kwako. Simama juu ya ahadi zilizo katika Biblia.

Mara ya kwanza unaweza kuwa na wakati mgumu kusikia Roho Mtakatifu wakati anapoongea na wewe. Usitarajie kusikia Mungu akiongea kwa sauti kubwa kwako. Ni mara chache yeye hufanya hivyo. Lakini atazungumza nawe moyoni mwako. Njia moja unayoweza kujifunza kumsikiliza vyema ni kuomba kila siku, “Roho Mtakatifu, nisaidie kukusikia leo wakati Unazungumza nami.” Labda tayari unajua jinsi anavyokuhukumu dhambi. Sasa kwa njia ile ile umsikilize akuongoze katika ukweli zaidi wa Mungu kila siku.

## C. Roho Mtakatifu hufanya nini katika maisha yako baada ya wewe kuwa Mkristo?

Kazi ya Roho Mtakatifu huanza tu wakati umeamua kuwa Mkristo. Yeye anataka kufanya zaidi ya kukuhukumu dhambi zako. Atakuwa rafiki yako wa kila wakati na msaidizi ikiwa utampa fursa hiyo.

### 1. Roho Mtakatifu hukusaidia kuwa Mkristo aliyefanikiwa

Kabla ya wewe kuwa Mkristo, roho yako ilikuwa imekufa. Sasa kwa kuwa umekuwa Mkristo, Roho Mtakatifu anaishi ndani yako. Yeye anataka kukuongoza kila siku na kukusaidia kuwa Mkristo mkomavu. Yeye anataka uanze kutumia mafundisho yake katika maeneo yote ya maisha yako. Unaweza kuanza kupata furaha ya wokovu Wake.

**Warumi 8:6-8 Biblia Takatifu –SUV**

**Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani.**
**7 Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. 8 Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.**

Sasa kwa kuwa umekuwa Mkristo, utajikuta unakabiliwa na maamuzi mengi katika miezi ijayo. Je! Utafanya kile unachotaka kufanya? Au utachagua kufanya kile Mungu anataka ufanye? Sehemu moja yako itatakaa kuendelea na tabia na mitazamo ya zamani. Katika maeneo mengine ya maisha yako, tamaa zako za zamani huenda zisitoweke mara moja. Lakini Mungu atakupa nguvu ya kuzishinda njia za zamani za dhambi ulizokuwa nazo na kuweka mitazamo na majibu mapya ambayo yanaashiria maisha ya Mkristo mwaminifu.

### 2. Roho Mtakatifu atakusaidia kuelewa ukweli wa Mungu

Sasa kwa kuwa umekuwa Mkristo, uelewa wako juu ya ukweli wa Mungu lazima uboreke. Biblia inaahidi kwamba Roho Mtakatifu atakuongoza katika ukweli wote.

Tazama Yohana 16:13. Ikiwa unataka kujifunza jinsi ya kufanikiwa, basi lazima ujifunze kutoka kwa Biblia mafundisho ambayo yatakuonyesha jinsi Mungu anataka uishi.

Biblia imejaa ushauri wa kutekeleza kuhusu jinsi ya kupenda watu wengine, kuonyesha fadhili, jinsi ya kukabiliana na hasira na hofu yako, jinsi ya kutumia kwa busara pesa na wakati wako, jinsi ya kuwa mzazi mwema, jinsi ya kushirikiana na watu wagumu, na mambo mengi zaidi. Lazima tupange kando ratiba ya kila siku ya kusoma Biblia na tumuulize Roho Mtakatifu atufundishe.

## 3. Roho Mtakatifu atakusaidia kupinga majaribu

Usishangae wakati Shetani anapokujaribu kutenda dhambi. Atafanya kila kitu kwa uwezo wake kuharibu uhusiano wako mpya na Mungu. Lakini hauhitaji kuogopa majaribu haya. Biblia imejaa ahadi ambazo Mungu anaahidi kutusaidia wakati majaribu yanapotujia. Sio lazima ushindwe na majaribu haya.

**Warumi 8:12-13 Biblia Takatifu- SUV**

**Basi, kama ni hivyo, ndugu, tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili, 13 kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyaua matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi.**

Mungu ameahidi kutengeza njia ya wewe kushinda wakati majaribu ya dhambi yanapokujia dhidi yako. Tazama 1 Wakorintho 10:13. Biblia inabainisha wazi kuwa Mungu atatumia kila jaribio na shida inayokuja kukuza ndani yako tabia na nguvu ya ndani inayoashiria Mkristo aliyefanikiwa. Tazama Yakobo 1:2-4 na Warumi 5:3-5. Roho Mtakatifu atakusaidia kukidhi mahitaji na matamanio yako kwa njia ya Mungu, kwa hivyo hautahitaji kujisalimisha kwa majaribu ya Shetani.

Lakini wacha tuwe wakweli. Hakuna mtu kamili. Hata Wakristo wakuu humfelisha Mungu na kuanguka katika majaribu kadhaa. Wakati huo Mungu huwa hakugusi kwa mgongo na kusema, “Hiyo ni sawa. Sitarajii uwe mkamilifu. Kuwa na bahati njema nzuri wakati mwingine.” Dhambi bado ni dhambi. Lazima ukiri dhambi zako, na uachane nazo. Shetani atakuhukumu na kujaribu kukufanya ughairi kuwa Mkristo. Lakini angalia kwa uangalifu ahadi iliyotolewa katika Warumi 8.

**Warumi 8:1-2, 4 Biblia Takatifu – SUV**

**Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. 2 Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. ... 4 ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho.**

Tuna jukumu la kuishi maisha matakatifu-kuondoa dhambi maishani mwetu na badala yake kufanya kile Mungu anatuambia katika Biblia kutenda. Kila Mkristo huwa anakabiliwa na majaribu, na moja ya majukumu makubwa ya Roho Mtakatifu ni kutuonya juu ya hatari iliyo mbele na kutuonyesha njia ya Mungu ya kushinda majaribu. Ikiwa tutapuuza sauti yake ya utulivu na kwenda mbele na kutenda dhambi, basi Roho Mtakatifu atatuhukumu kwa dhambi yetu. Atatusaidia kukua kupitia kwa mafanikio yetu na kushindwa kwetu ikiwa tutamwacha atufundishe.

Somo hili la kushinda majaribu limefunzwa kwa undani zaidi katika kazi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* inayoitwa, **Majaribu**.

## 4. Roho Mtakatifu huzaa matunda yake maishani mwako

Sehemu kadhaa katika Agano Jipya zinaelezea mchakato wa kuwa Mkristo aliyefanikiwa kama kitendo cha kujiondo kuwa mtu wa kale na kuwa mtu mpya. Mungu anataka uwe mtu mpya kabisa. Je! Hiyo inamaanisha lazima uache kuwa wewe mwenyewe, na kuwa mtu mwingine? Hapana. Inamaanisha kuzivua tabia na mitazamo mibaya na kuzibadilisha kwa sifa na tabia ambazo zitakufanya uonekane zaidi kama Yesu. Inamaanisha "kuvaa" mitazamo na tabia ambazo Yesu alikuwa nazo wakati aliishi duniani. Je! Sifa hizi za kiungu ni zipi?

Wagalatia 5:22-23 hutoa orodha ya sifa tisa na kuzieleza kama "tunda la Roho." Ikiwa utampa Roho Mtakatifu uhuru wa kufanya kazi katika maisha yako, basi utaona sifa hizi zikiongezeka maishani mwako zaidi na zaidi kadri wiki zinavypita.

**Wagalatia 5:22-23 Biblia Takatifu – SUV**

**Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, 23 upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.**

Lazima ushirikiane na Roho Mtakatifu ikiwa unataka kuona sifa hizi zikikua katika maisha yako. Mabadiliko hayatakuja tu mara moja kwa wewe kwenda kanisani tu. Wagalatia 5:24-25 inaeleza wazi ukweli huu.

**Wagalatia 5:24-25 Biblia Takatifu – SUV**

**Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. 25 Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho.**

Tafuta fursa kila siku kuonyesha "tunda" hili katika shughuli zako za kila siku. Unapokuwa nyumbani, wakati wa kula, kazini, unapopumzika baaada ya kazi, au unapofanya kitu maalum, jaribu kuweka masikio yako yawe makini kumsikiliza Roho Mtakatifu. Atakuongoza kila siku ili "tunda" hili liwe na usemi dhabiti wa kiungu katika maisha yako kama ilivyokuwa katika Yesu.

## 5. Unaweza kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu

Agano Jipya linazungumza katika sehemu nyingi kuhusu karama tofauti ambazo Mungu huwakirimia watoto wake. Moja ya karama hizi mara nyingi huitwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sio makanisa yote ya leo hukubaliana kuhusu swala la karama hii ni nini au jinsi inapaswa kutumiwa leo. Ikiwa una nia ya kupokea karama hii, au ikiwa Wakristo unaoshirikiana nao wanakuhimiza uombe ubatizo wa Roho Mtakatifu, basi tulia kwanza na ujibu maswali haya:

Ni kwa nini ninataka ubatizo wa Roho Mtakatifu?

Nitafanya nini na karama hii ikiwa Mungu atanipa?

Ikiwa huwezi kujibu maswali haya, basi unahitaji kusoma Biblia kwanza na ujue Mungu anasema nini kama majibu ya maswali haya. Mungu hawapi watoto wake karama hii ili waweze kuweka kombe lingine kwenye rafu yao na kusema, "Ndiyo, niangalie! Nimeshinda kombe jingine kubwa!"

Mungu hutoa karama za kiroho kwa watoto wake kwa sababu mbili za msingi:

1. Kutusaidia kukuza uhusiano wa karibu na Yeye.
2. Kutuwezesha kufanikiwa zaidi katika kazi aliyotupa kufanya tunapoendelea kufanya huduma aliyotuitia kufanya.

Tutaangalia tena maswala haya mawili katika sehemu inayofuata ya sura hii, lakini hivi sasa hebu tuangalie umakini wetu juu ya jinsi maswala haya yanahusiana na Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

### a. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni nini?

Wakristo wengine huchangayikiwa kuhusu karama hii kwa sababu wanashindwa kujua nini Biblia inasema juu yake. “Je! Unaye Roho Mtakatifu tayari?” wao huuliza. “Je! Umejazwa na Roho?” Katika visa vyote viwili labda wanamaanisha, “Je! Umepokea karama tunayoiita ubatizo wa Roho Mtakatifu?”

Karama hii si sawa na wokovu. Wokovu ni karama kuu kuliko zawadi zote za Mungu kwetu. Na alilipia kwa bei ghali karama hiyo! Yesu alikufa msalabani ili tuweze kupokea bure karama ya wokovu. Wakati wa wokovu, Roho Mtakatifu huja na kuishi ndani ya mtu. Kwa hivyo wakati mtu anapouliza, “Je! Unayo Roho Mtakatifu?” Mtu yeyote ambaye ni Mkristo wa kweli anaweza kusema kwa uaminifu na kwa ujasiri, “Ndio.”

Kwa hivyo ubatizo wa Roho Mtakatifu ni nini? Unahitaji kusoma Biblia mwenyewe na kumwomba Roho Mtakatifu akuongoze katika ukweli kuhusu karama hii.

Hivi ndivyo Wakristo wengine wanavyojibu swali hilo. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni zawadi ya kiroho iliyotolewa na Mungu kwa watoto wake. Matendo sura ya pili katika Biblia inasimulia juu ya mara ya kwanza Mungu alitoa karama hii kwa watoto wake baada ya kufufuka kwa Yesu. Katika maelezo aliyotoa Petro kwa umati siku hiyo alinukuu kutoka kwa Yoeli 2:28-32 ambayo ilitabiri jinsi Mungu atakavyomimina Roho Wake kwa kila mtu. Karama hii haijahifadhiwa kwa viongozi wachache wa kiroho wa wasomi. Inapatikana kwa watoto wote wa Mungu.

Katika Matendo 2 na mahali pengine kadhaa katika Agano Jipya, ushahidi wa kwanza wa nje wa mtu anayepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kwamba walizungumza kwa lugha ambayo kamwe hawakuwa wamewai kujifunza. Kila mtu alianza kuomba na kumsifu Mungu kwa maneno ambayo hakukuwa amewai kujifunza. Roho Mtakatifu alikuwa akiongea. Kila mtu ilibidi amruhusu Roho Mtakatifu kudhibiti hotuba zao.

Je! Hiyo ndiyo yote iliyopo khuhusu karama hii- kusema tu maneno ambayo hujawahi kujifunza? Wakristo wengine husema, “Ndio.” Wengine hujibu, “Hapana, kuna mambo zaidi ya karama hii.” Zaidi kiasi gani? Wanasema kwamba kuzungumza kwa lugha isiyojulikana ni onyesho la nje la karama hii ya kiroho. Ni zawadi ya kiroho, na ni kielelezo chake kikuu kilicho katika roho zetu ambazo haziwezi kuonekana. Je! Karama hii ndiyo tiba ya haraka kwa shida zako zote za kiroho? Hapana. Kwa kweli, hakuna zawadi yoyote ya Mungu itakayotatua shida zako mara moja.

Ubatizo wa Roho Mtakatifu sio karama ya kukupa msisimuko mkuu wa kihisia— “kulewa Mungu.” Wakristo wengi hutambua kwamba karama hii inaleta furaha kubwa katika maisha yao. Furaha ni faida ya kupendeza ya karama hii, lakini sio kusudi kuu la Mungu kutoa karama hii kwa watoto Wake.

Mungu huwapa watoto wake zawadi hii ili kujenga maisha yao ya kiroho. Ukuaji huu wa kiroho unapaswa kuathiri moja kwa moja maisha yetu ya kila siku na wengine.

Inaweza kuwa vigumu kupata ufafanuzi wa ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao Wakristo wote watakubaliana nao. Vivyo hivyo ni vigumu kutoa ufafanuzi kamili wa upendo ni nini. Upendo ni zaidi ya kubusu, kukumbatiana, hisia za mapenzi, na mawazo mema. Ni zaidi ya vitendo vya mwili. Lakini ikiwa unampenda mtu kweli, utaonyesha kupitia matendo na hisia zako. Upendo wa kweli huathiri mawazo yako, lakini ni zaidi ya mawazo ya kupenda.

Ikiwa kweli unataka kujua upendo ni nini, lazima uupokee. Kadri unavyoupokea, ndivyo utakavyouelewa vizuri ni nini. Ndivyo ilivyo pia juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Huwezi kuuelewa kabisa akilini mwako mpaka utakapopata uzoefu katika roho yako na maisha yako yote.

## b. Utafanya nini na karama hii ikiwa Mungu atakupa?

Mungu ni Baba mwenye busara, na hatatoa ovyo ovyo vipawa vyake kwa watoto wake na kuwaacha wavitumie vibaya. Anatupenda sana na anataka kuonyesha upendo wake kwetu. Ana hamu ya kutoa karama za kiroho kwa wale ambao wanataka uhusiano wa ndani zaidi na Yeye. Mungu kamwe hatalazimisha karama Zake kwako. Ikiwa hutaki ubatizo wa Roho Mtakatifu, hatakupa. Kwa nini basi Mkristo atake kupokea karama hii? Itakufaidije?

Je! Biblia inasema nini kitatokea kwa Mkristo aliye na karama hii? Matendo 1:8 inatoa faida moja kwa wale wanaopokea karama hii. Watapokea nguvu ya kushuhudia juu ya Kristo na nguvu Yake ya kuokoa kwa wasio Wakristo.

Njia moja ya msingi ambayo karama hii inapaswa kukuathiri ni kukusaidia kukuza uhusiano wa karibu na Mungu. Paulo anaandika juu ya sehemu muhimu ya karama hii katika maisha yake ya maombi. “Namshukuru Mungu ya kuwa nanena kwa lugha zaidi ya nyinyi nyote.” (1 Wakorintho 14:18 Biblia Takatifu –SUV)

Zawadi ya kunena kwa lugha — lugha ambazo hujajifunza — inaweza kuwa nyenzo kubwa ya kukusogeza karibu na Mungu. Lakini jukumu liko juu yako kutumia vyema karama hii. Kwa sababu una karama hii haimaanishi wewe ni bora kuliko Wakristo wengine. Ikiwa karama hii haina athari nzuri juu ya uhusiano wako na Mungu, basi unashindwa kuitumia karama hiyo vyema.

Karama hii inapaswa kujenga ndani yako hamu kubwa ya kukaa karibu na Mungu. Inapaswa kukuchochea uondoe mitazamo na mazoea ya dhambi na uvae tabia za kiungu. Zawadi hii inapaswa kuwa na athari kubwa katika uhusiano wako na watu wengine. Wanapaswa kuona zaidi ya upendo wa kweli na furaha ambayo Mungu amekuletea maishani mwako. Ikiwa wewe si Mkristo aliye na upendo zaidi ukiwa na karama hii, basi unashindwa kuitumia vizuri.

Unapopokea karama ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, usishangae ikiwa hakuna mabadiliko ya haraka yanayotokea katika maisha yako. Lakini karama hii inapaswa kukupa nguvu ya kukua na kuwa zaidi kama Kristo. Kwa sababu tu umepata seti mpya ya mpira wa tenisi kama zawadi haikufanyi uwe mchezaji wa tenisi stadi. Lakini huwezi kuwa mchezaji stadi wa tenisi ikiwa huna raketi ya tenisi. Vivyo hivyo, karama hii kutoka kwa Mungu itakufungulia fursa nyingi za ukuaji wa kiroho na huduma.

Mabadiliko mengine ambayo karama hii inapaswa kuleta maishani mwako ni kukusaidia kukuza tabia itakayofanya uwe mtu wa kupenda kufunzwa. Utataka kujifunza zaidi juu ya Mungu na jinsi unavyoweza kumtumikia vyema. Ikiwa kiburi na uasi na tabia ya "Najua yote" kipo katika maisha yako, basi unashindwa kutumia karama hii kwa njia ambayo Mungu anataka uitumie.

### c. Unawezaje kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu?

Hakuna kitu chochote unaweza kufanya ili kupokea karama hii kutoka kwa Mungu. Huwezi kufanyia kazi wokovu au karama yoyote ya Mungu. Mungu hutoa karama Zake kwa watoto Wake. Yeye ndiye hufanya maamuzi. Inakubalika kwako kumjulisha Mungu mahitaji yako. Ikiwa kwa mfano mtoto atawaambia wazazi wake, "Sitaki zawadi ya vitabu vyovyote wakati wa Krismasi." Je! Unafikiri watasikiliza yale mtoto alisema? Bila shaka watamsikiza. Wanampenda mtoto wao na wanataka kumpa zawadi ambayo itamsaidia, na pia inayompendeza.

Mungu hatalazimisha karama Zake kwa watoto Wake. Kwa upande mwingine, huwezi kumlazimisha kukupa karama hii. Wakati mwingine watoto huendelea kuuliza na kuuliza, mpaka wazazi hatimaye wanasalimu amri na kuwapa kile wanachotaka ili tu kuwa na amani nyumbani. Lakini Mungu huwa hashinikizwi kuchukua maamuzi.

Ikiwa unataka karama yoyote kutoka kwa Mungu, basi fanya kipaumbele chako cha kwanza na kikubwa kiwe kumkaribia Yeye. Jitahidi kutii amri kuu mbili katika Biblia. Je, ni nini kinaweza kuwa muhimu zaidi maishani kuliko kutii amri hizi mbili? Tazama Marko 12:28-31.

Je! Unamwona wapi Yesu akiomba kwa Mungu Baba na kusema, "Tafadhali, nipe karama zaidi leo." Je! Wewe huenda kwa wale unaowapenda na kusema, "Nataka zawadi kutoka kwako leo." Hiyo sio njia ya kujenga urafiki wa kina. Badala yake, tafuta njia ambazo unaweza kufanya kile ambacho Mungu amekuambia ufanye. Ikiwa unakabiliwa na hali ambayo hauna nguvu ya kufanya kile unachojua Mungu anataka ufanye, omba msaada Wake. Atakusaidia. Ikiwa unahitaji upendo zaidi, mwombe Mungu akusaidie umpende huyo mtu mgumu.

Ikiwa unataka kumkaribia Mungu, mwambie. Atasikiliza. Ikiwa unataka kuwa na ufanisi zaidi kuwahubiria wasio Wakristo, mwambie Mungu. Ikiwa unataka nguvu zaidi ya kiroho maishani mwako, mwombe Mungu akusaidie. Usitumie wakati wako wote kumwuliza Mungu karama za kiroho. Badala yake, tumia muda wako kumsogelea Mungu. Yeye hupenda kuwamiminia karama Zake wale ambao wanaweka vipaumbele vyao kwa njia sawa.

## 6. Hutoa karama za Roho Mtakatifu

Roho Mtakatifu anataka kutupa nguvu ya kuwa Wakristo waliofanikiwa. Anataka kutuandaa kwa huduma. Wazo la Mungu la huduma sio tu kuwa mhubiri au mmishonari. Anataka kila mmoja wa watoto Wake amfanyie kazi pale pale walipo. Hakuna aliye mdogo sana kutumiwa na Mungu. Atakuongoza, lakini lazima uende kazini. Unapofanya kazi anayoweka mbele yako, Yeye atakupa msaada unaohitaji.

Baadhi ya karama za Roho Mtakatifu zinapaswa kutumiwa katika huduma ya umma. Wakorintho wa kwanza sura ya 12 inaelezea vipawa hivi na jinsi ya kutumiwa.

Warumi 12 na Waefeso 4 inaelezea karama zingine kadhaa ambazo Roho Mtakatifu huwapa Wakristo. Zawadi hizi zinapaswa kutumika katika maisha yetu ya kila siku na kazi. Warumi 12:6 na Waefeso 4:7 zinasema kwamba Mungu amempa kila Mkristo angalau karama moja ya kiroho. Waefeso 4:12-13 inaelezea kusudi la karama hizi.

**Waefeso 4:11-13 Biblia Takatifu –SUV**

**Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; 12 kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; 13 hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo.**

Petro wa Kwanza 4 pia huorodhesha karama zingine za Roho Mtakatifu. Iwe una karama ya kufundisha, kuonyesha huruma, imani, uponyaji, usimamizi, au kuhubiri, Mungu anataka utumie zawadi hiyo kusaidia ufalme wake ukue. Anataka utumie karama hiyo kumletea Mungu utukufu, sio wewe mwenyewe.

Roho Mtakatifu anataka kuwa na nafasi maalum katika maisha yako. Ni wewe unayechagua ni kiasi gani atakuwa na ushawishi katika maisha yako ya kila siku. Ukipuuza msaada Wake, utakabiliwa na kushindwa mara kwa mara. Jambo muhimu zaidi unaloweza kufanya ni kumkaribia Mungu kila siku. Unaposoma Biblia, mwombe Roho Mtakatifu akufundishe. Tafuta njia za vitendo za kuelezea matunda ya Roho Mtakatifu katika shughuli zako za kila siku. Jifunze kumsikiliza wakati anazungumza nawe moyoni mwako. Barabara hii ambayo Mungu amekuwekea itasababisha mafanikio ya kweli.